# BWANA YESU UNIOKOE

BY: Deogratius Kalolela
Arusha




2. Duniani sijamuona, awezaye kunifariji x2
Nikiyatazama maovu duniani yanavyoongezeka,
Si mkubwa wala mdogo anayezitafakari nyakati
Hakuna anayefikiri kwamba karibu Yesu unakuja
Ndio maana ninakuja nakukiri kwamba wewe Yesu ni Bwana

3. Mara nyingi nimekutesa, Kwa matendo yangu maovu x2
Sikujua nafanya nini nilipokuwa natenda mabaya
Sikujua nalichafua hekalu la Roho Mtakatifu
Ingawa nalikuchukiza kwa matendo yangu mengi maovu
Bado wewe ukanipenda na ukaendelea kunitunza vyema

4. Nisamehe Mwokozi wangu, Moyo wangu unakukiri x2
Wewe ni mchungaji wangu, kamwe sitapungukiwa na kitu,
Wewe ni njia ya wokovu, ya kwenda mbinguni kwa Baba Yetu,
Wewe ni chakula cha kweli, wewe ni kinywaji cha Roho zetu,
Yesu wangu ninaahidi, ninakupa Moyo na mwili wangu wote

*Copied By: G.M.Kombo*
*Capella Software!*
*"gevakom@yahoo.com"*